

10/12/2020

Familia na wafanyakazi wa RPS 205,

Imekuwa mwezi mmoja tangu tufungue tena shule zetu na kuanza mwaka huu tena ambao haujawahi kutokea. Bado tunaendelea kukerebisha kawaida yetu mpya ya barakoa, hali ya kusimama umbalimbali, barabara ya njia moja ndani ya shule, na mishale ambao inayoonesha njia ya kufuata sakafuni.

Idara ya Afya ya Kaunti ya Winnebago imekuwa sawa na wazi katika ujumbe wake kwa wasimamizi na wafanyakazi: wanafunzi na wafanyakazi wanafanya kazi bora ili kutunza kila mmoja salama. Hadi sasa, COVID-19 haisambazwi ndani ya shule zetu. Tunajuwa kuwa kwa sababu ya njia ya kufuatiliya mawasiiano ya karibu na uchunguzi wetu wa kina na Idara ya Afya na wafanyakazi wetu wauguzi wa shule.

Wakati kiwango cha Kaunti ya Winnebago cha watu ambao wanapimwa kuwa na ugonjwa inapanda juu, Kiwango cha ugonjwa katika Shule ya Umma ya Rockford ni chini ya asilimia 1 kwa wafanyakazi na, ni asilimia .5 kwa wanafunzi. Ripoti za vyombo vya habari huorodhesha kila kesi mpya katika shule zetu, na hiyo inaweza kutisha. Lakini kumbuka kwa kila kesi ya ugonjwa shuleni, watu mia chache au hata elfu hawaathiriwi.

Pamoja na habari njema ni kuchanganyikiwa. Tunaendelea kuweka shule zetu salama, na kwa kweli, tunatuma wanafunzi wote na wafanyakazi nyumbani ambao wanaonesha dalili zozote ya COVID-19. Kwa kila mwanafunzi yeyote ambao anarudishwa nyumbani kwa kuonesha dalili, na ndugu wa mwanafunzi huyo hurudishwa nyumbani pia kwa karantini kama njia ya tahadhali.

Njia hii haijulikane ku watu. Lakini inahitajika kulingana na maelekezo kutoka Idara ya Afya ya Kaunti ya Winnebago, Idara ya Afya ya Umma ya Illinois na Vituo vya Udhhibiti na Kuzuia Ugonjwa. Tunaendelea kutii mwongozo huo kwa tahadhali nyingi. Hatuwezi kuchukua hatari ya kuchunga mwanafunzi na mfanyanakazi mgonjwa ndani ya shule.

Wakati msimu wa baridi na homa unakaribia na hali ya hewa kuendelea kuwa baridi, tunatarajia wanafunzi na wafanyakazi wataendelea kuonesha dalili za homa na mafua – na Virusi ya Corona. Tunaendelea kuwa waangalifu na kuweka usalama kwa wanafunzi na wafanyakazi mbele.

Tafadhali, endelea kufuatilia wanafunzi na wanamemba wa familia kwa dalili zinazowezekana za COVID-19: homa, baridi, kikohozi, upungufu wa pumzi au shida ya kupumua, mchoko, maumivu ya misuli au ya mwili, maumivu ya kichwa, kupoteza ladha au harufu, vidonda kooni, msongamano au mafua, kuhara, na kichefuchefu au kutapika.

Tunawasiliana mara kwa mara na Idara ya Afya ya Kaunti ya Winnebago, na maafisa wanakubali kwamba majifunzo ya jengoni ni kipaumbele kwa jammii na familia zetu. Tunaendelea kugawanya habari mpya Wakati tunaipata. Tunashukuru kwa mawasiliano na ushirikiano wenu Wakati huu.

Kwa dhati,

Ehren Jarrett
Superintendent
Rockford Public Schools

